

NG'OMBE KUKAMATWA HIFADHINI

# Wafugaji waiangukia\*

## Serikali isiuzwe



**"Tunaelekea katika siku za haki za binadamu, wananchi wanaotege-me mifugo na wanaokumbwa na ukame, wana hall mbaya tuwa-hurumle,"**

Ole Ngurumwa

**Baada ya mifugo yao kukamatwa ikiwa ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, wafugaji wameomba Serikali isiipige mnada.**

Mussa Juma, Mwananchi  
mjuma@mwananchi.co.tz

**Arusha.** Ng'ombe 870 wamekamatwa wakiwa wamefuata malisho ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kutokana na maeneo mengi ya malisho ya mifugo kuathirika na ukame.

Kutokana na hali hiyo, baa-dhi ya wafugaji na watetezi wa jamii ya wafugaji wameomba Serikali kutowapiga mnada ng'ombe hao, kwa madai kuwa hali hiyo inatokana na kupungua maeneo ya malisho katika tarafa ya Loliondo.

Mkuu wa hifadhi hiyo, Kamishna Msaidizi Mwandam-

izi Izumbe Msindai alikiri jana kukamatwa mifugo hiyo na taratibu za kisheria zinaende-lea.

Akizungumza na *Mwananchi*, Mkurugenzi wa Shirika la kui-nua na kusaidia maisha ya wafugaji nchini (PALISEP), Robert Kamakia alisema wafugaji wa Loliondo wanapata wakati mgumu kupata malisho kuto-kana na ukame.

"Tunaomba Serikali na Hifa-dhi ya Taifa wa Serengeti isii-uze hii mifugo, waangalie hali ya sasa kuna kiangazi Loliondo, mifugo inakufa kwa kukosa malisho, kilichotokea ni mifugo kukimbilia hifadhini isife.

"Unajua kwa hali ya ukame na kukosa malisho hata ng'ombe wenyewe wanaweza kutoroka usiku kwenye mazizi na kufuata majani, sasa hili tunaishi Seri-ki kuwaonea huruma hawa wafugaji," alisema.

Alisema mifugo hiyo imehi-fadiwa katika eneo la Org'oswa ndani ya Hifadhi ya Serengeti ikisubiri hatua zaidi.

Akizungumza na *Mwanan-chi*, Mratibu wa Mtando wa watetezi wa haki za Binadamu nchini (THRDC), Onesmo Ole Ngurumwa ameomba Serikali kutafakari hatua za kuchukua ambazo hazitaathiri uchumi na maisha ya wananchi wenyewe mifugo hiyo.